# ura ya 28: Mafumbo kama Mkakati wa Mawasiliano ka *Diskosi* Kuhusu UKIMWI katika Lugha ya Ekegusii

*Carren Nyandiba*
cnyandiba@yahoo.com

## gulizi

la Virusi Vya Ukimwi (VVU) na UKIMWI lingali atatiza wataalamu wa tiba na watafiti katika nyanja i. Hii ni kwa sababu tiba ya ugonjwa huu haijapatikana. , ingawa idadi ya watu wanaokufa kutokana na makali ya WI imepungua, ugonjwa wa UKIMWI ungali unaathiri zote za ulimwengu. Mazungumzo kuhusu UKIMWI, hususani mazungumzo ya nasaha na ushauri, a masuala ambayo ni nyeti mno. Baadhi ya masuala i kujamiiana, sehemu za siri, jinsi ya kuishi na virusi, na izi ya kondomu. Tafiti zimeonesha kwamba, kuna lugha na miiko kuhusu masuala nyeti; na, Kwa hiyo, gumzo yanayogusia masuala hayo hufanywa kwa lugha na isiyo na mafumbo wala tasfida. Kwa upande ne, kuna lugha ambazo huwekea mwiko masuala yanachukuliwa kuwa ni nyeti. Kwa hiyo, mazungumzo mambo ambayo ni mwiko hufanywa kwa lugha ya o, tasifida, methali, na mbinu nyinginezo punguza' aibu, hasa mazungumzo hayo yanapofanywa miktadha ya watu wengi. *Ekegusii*, lugha ngumzwa na*Abagusii* (Jamii ya Wabantu wanaoishi neo la Kusini Magharibi mwa Kenya) ni mojawapo ya mbazo zina mwiko kuhusu maneno yanayohusu kitendo miiana, sehemu za siri na haja za kibayolojia. Kwa vile mzo na nasaha kuhusu VVU/UKIMWI hayawezi a bila kutaja sehemu za siri, kitendo cha kujamiiana na ya kondomu, sura hii inajadili mafumbo

yanayotumika katika mijadala hiyo. Sura inalenga kujibu maswali yafuatayo: Je ni mafumbo gani yanayotumika katika kuelezea sehemu za siri? Ni mafumbo gani yanatumika katika kueleza kitendo cha kujamiiana na matumizi ya kondomu? Je mafumbo hayo hubadilika kiwakati?

Data zinazounda mjadala wa sura hii zilitokana na utafiti uliohusisha washauri na washauriwa kutoka jamii ya Abagusii. Hii ni kwa sababu utafiti ulihusu matumizi ya lugha ya unasihi kuhusu VVU/UKIMWI miongoni mwa Abagusii. Utafiti ulifanyika katika hospitali zilizoko katika kaunti za Kisii na Nyamira, katika eneo la Nyanza, nchini Kenya. Uchunguzi ulijumuisha hospitali tatu ambazo ni hospitali ya Masaba, Nyansiongo na Tabaka. Katika kila hospitali, mazungumzo katika mkutano mmoja wa ushauri yalirekodiwa kwa minajili ya sura hii. Mazumgumzo hayo yalitumika katika kuainisha mafumbo katika kategoria mbalimbali. Kategeoria zilizotumika katika sura hii ni tano, yaani mafumbo kuhusu sehemu za siri, kuhusu kitendo cha ngono, kuhusu kondomu, kuhusu kitendo cha ngono, kuhusu VVU/UKIMWI na mafumbo kuhusu watu wanaoishi na VVU/UKIMWI.

**Dhana ya Mafumbo**

Dhana ya mafumbo imejadiliwa na wataalam mbalimbali kwa kuzingatia nadharia na mielekeo tofauti (Lakoff na Johnson, 1980; Sopory na Dillard, 2002; Erkert na McConnell-Ginnet, 2003; Coulmas 2005 na Steen 2008). Steen (khj) anafasili mafumbo kuwa ni njia ya kuelewa kitu kimoja kwa kutumia kitu kingine. Maoni ya Steen (khj) yanaendana na ya Sopory na Dillard (2002) wanaodai kwamba kitu kinachotumiwa huwa ni 'asilia', ilhali kile kinachoelezea ni 'kilengwa'. Kwa mfano, katika fumbo 'babangu ni simba' baba ni asilia na simba ni kilengwa. Kwa upande mwingine, McGlone (2007) anasema kwamba uelewaji wa mafumbo unategemea ujuzi wa msikilizaji wa vitu vilivyotumiwa katika fumbo. Kwa hiyo,

iwapo fumbo litatumia vitu ambavyo msikilizaji anavielewa na kuvitambua ataweza kuelewa maana ya fumbo hilo kuliko iwapo fumbo litatumia vitu asivyovifahamu. Hata hivyo, kulingana na Bowdle na Gentner (2005), kuna baadhi ya mafumbo ambayo hayawezi kueleweka haraka kwa vile yanahusiana na taaluma mahususi. Ili kuelewa mafumbo kama hayo, msikilizaji huhitajika kuelewa mambo fulani kuhusu taaluma hiyo.

Kwa mujibu wa Steen (2008), katika uchunguzi wa mafumbo, mbali na kuelewa vipengee vya kiisimu vya fumbo, ni muhimu pia kuelewa kipengee cha mawasiliano cha fumbo hilo. Anaainisha mafumbo katika kategoria mbili, mafumbo makusudi na mafumbo yasiyo makusudi. Mafumbo ya makusudi hutolewa na msemaji fulani akiwa na lengo la kumwathiri msikilizaji kwa njia fulani. Mafumbo yasiyo makusudi hutumiwa na msemaji fulani bila yeye kulenga kumwathiri msikilizaji kwa njia yoyote mahususi. Hali hii ndiyo hutofautisha mafumbo makusudi na yale yasiyo makusudi. Steen (keshatajwa) anaorodhesha majukumu matatu ya mafumbo. Nayo ni: jukumu la kiisimu (kuongezea msamiati katika mfumo wa lugha), jukumu la kinadharia (kujenga nadharia kutoka kwa mafumbo), pamoja na jukumu la kimawasiliano (kutoa mwelekeo mpya wa kuelewa jambo na hivyo kubadili maoni ya msikilizaji).

Sura hii inajadili mafumbo kwa msingi wa jukumu la kimawasiliano. Inajadili jinsi mafumbo yanavyotumiwa katika kuwasilisha ujumbe kwa njia inayoweza kueleweka na kukubalika kwa washiriki wa mazungumzo ya VVU/UKIMWI. Kwa mujibu wa Cain na wenzake (2011), watu huongozwa na vipengee mbalimbali wanapowasiliana. Kipengee muhimu katika mawasiliano ni matumizi ya lugha isiyoleta aibu kwa washiriki wa mazungumzo hayo. Matumizi ya mafumbo ni njia mojawapo ya kupunguza aibu kwa wasikilizaji katika

mawasiliano (Coulmas, 2005; Cain na wenzake, 2011). Sura hii inachanganua mafumbo kuhusu sehemu za siri za wanaume, sehemu za siri za wanawake, kuhusu ngono, kuhusu VVU/UKIMWI na kuhusu matumizi ya kondomu.

**Mafumbo kuhusu Sehemu za Siri za Mwanaume**

Sehemu hii inajadili mafumbo kumi na moja (11) yanayotumika kutaja sehemu ya siri ya mwanaume katika Ekegusii. Mafumbo hayo yamegawanya katika kategoria mbili, yaani mafumbo ya kiasilia na yale yanayotokana na maneno ya mkopo, kama jedwali lifuatalo linavyoonesha:

| **Mafumbo ya kiasilia** | **Maana** | **Mafumbo yanayotokana na maneno ya mkopo** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| **Obosacha** | Uume | **Ekaramu** | Kalamu |
| **Omogaka** | Mzee | **Epensiri** | Penseli |
| **Esese** | Mbwa | **Echuma** | Chuma |
| **Ekeranya** | Kiboko | | |
| **Omote** | Mti | | |
| **Ritimo** | Mkuki | | |
| **Omoswago** | Mchi | | |
| **Obokombe** | Jembe | | |

Chanzo: Utafiti (2017).

Ijapokuwa sehemu ya siri ya mwanaume ina majina ya kuitajia katika Ekegusii kama vile **emboro** (mboo) au **ekemincha** (mkia), katika mazungumzo ya hadharani majina hayo yalikwepwa; badala yake, mafumbo kama vile **obosacha** na **omogaka** hutumika. Kwa mujibu wa Akama na Maxon (2006), Abagusii wanaongozwa na sheria zinazooitwa **chinsoni** (sheria za heshima), ambazo zinawazuia kutaja sehemu za siri na kitendo cha ngono hadharani. Kwa hiyo, kukwepa kutaja

sehemu ya siri kwa jina lake ni hali inayotokana na **chinsoni** ambazo lazima mzungumzaji azingatie.

Katika kategoria ya mafumbo yanayotokana na maneno ya kiasili, mafumbo yaliyotumiwa huambatana na majukumu mbalimbali ambayo sehemu hiyo imetengewa. Abagusii, kama zilivyo jamii nyinginezo za kuumeni, inawapa wanaume jukumu la kuongoza jamii na familia (Akama na Maxon, 2006; Nyakoe, 2011). Nguvu alizopewa mwanaume na jamii zimeweza kujitokeza kupitia jinsi mwili na viungo mbalimbali vinafafanuliwa. Mfano wa umuhimu wa sehemu hiyo unaonekana katika matumizi ya fumbo **omogaka** (mzee) kutaja sehemu ya siri ya mwanaume. Katika kutumia fumbo hilo, sehemu hiyo imepewa jukumu la kiongozi wa mwili wa mwanaume na kiongozi wa jamii (inayojumuisha mke na watoto). Katika jamii ya kiasili ya Abagusii, **omogaka bwo omochie** (mzee wa familia) alikuwa muhimu sana, kwani maamuzi yote yalifanywa naye. Aidha, watoto na wanawake walikuwa chini yake (Akama na Maxon, 2006). Kwa hiyo, sehemu ya siri ya mwanaume inapopewa jina **omogaka** (mzee), hupewa nguvu na mamlaka sawa na yale ya mzee katika familia. Kwa upande mwingine, fumbo hili hutoa taswira ya mzee mwenye ndevu; yumkini, ulinganisho huu na sehemu ya siri huenda unatokana na jinsi sehemu hiyo inavyoonekana.

Umuhimu wa sehemu hiyo unakolezwa na fumbo **obosacha** (uume), kwamba hiyo ndiyo mojawapo ya sifa za uume wa mwanaume. Katika Ekegusii, **obosacha** humaanisha ujasiri, nguvu na mamlaka. Dhana hii inatumika katika semi kama vile katika mfano ufuataao:

**Tema ingo torore obosacha bwao**
Hebu jaribu tuone uume wako.

Mfano huu umetolewa katika semi zinazotumika katika mazungumzo ya kila siku miongoni mwa wanajamii. Msemo kama huu hutumika ili kudhihirisha kwamba mwanaume ni nguvu, ujasiri na haogopi chochote. Kwa hiyo, kuiita sehemu ya siri ya mwanaume **obosacha** (uume) inaonesha umuhimu wa sehemu hiyo, sio tu kwa wanaume bali pia kwa jamii kwa ujumla. Fumbo hili limetokana na sababu kwamba sehemu hii ndiyo hutoa mbegu za uzazi, kwa hiyo ina umuhimu katika kuendeleza vizazi.

Lugha ya ngono na sehemu za siri inaweza kubainishwa kama rejista maalum (Kobia, 2008). Uchunguzi kuhusu lugha ya ngono miongoni mwa wanajamii ya Abagusii ulionesha kwamba wanaume wanachukuliwa kama watendaji huku wanawake wakichukuliwa kama wapokeaji tu wa huduma kutoka kwa wanaume. Hii lilijitokeza katika matumizi ya mafumbo **ekeranya** (kiboko), **ekaramu** (kalamu), **epensiri** (penseli) na **omote** (mti). Katika kutumia fumbo **ekeranya** (kiboko), jukumu la sehemu ya siri yamwanaume linakuwa ni la kumwadhibu mwanamke. Hii inaonesha kwamba ngono inaweza kutumika katika kutimiza majukumu zaidi ya moja. Jukumu la kwanza ni uzazi; lingine, kulingana na fumbo hili, ni kumwadhibu mwanamke. Jukumu hili lilidhihirika katika mazungumzo ya unasihi katika tamko lifuatalo:

Msh: **Kamorache abasacha more aiga, timogoita mokungu onde bwensi biranya ense yabeire bobe. Gose kerabetererie, beka esogisi gaki.**

Tafadhalini wanaume wote mlioko hapa, msichape mwanamke yeyote viboko, dunia imeharibika. Lakini ikibidi, vaa soksi tafadhali.

Muktadha: Mazungumzo haya yalitokea katika mkutano wa unasihi, ambapo Mshauri aliwaonya wanaume dhidi ya kufanya ngono kiholela.

Mfano huu unarejelea kufanya ngono kiholela kama kuwachapa wanawake viboko. Fumbo hili linafananisha sehemu ya siri ya mwanaume na **ekeranya** (kiboko), huku kufanya ngono kukilinganishwa na kuchapa kwa kiboko. Yawezekana pia kuwa fumbo hili lilitokana na umbo la sehemu hiyo, yaani kutokana na kulinganisha umbile la sehemu ya siri na kiboko ambacho hutengenezwa kwa kijiti au mti. Mafumbo yanayokaribiana na **ekeranya** ni **omoswago** (mchi) na **omote** (mti). Mafumbo haya yametokana na kufanya ulinganisho wa sehemu hiyo na mchi au mti. Kwa hiyo, kitendo cha kufanya ngono kinafananishwa na kutwanga nafaka kwa kutumia kinu na mchi, au kuangukiwa na mti.

Fumbo **ritimo** (mkuki**)** kama vile **ekeranya** (kiboko) lilitumiwa katika kuonya wanaume kutofanya ngono kiholela kama mfano ufuatao unavyoonyesha.

Msh: **Tobaise gokang'a buna naye egiata okobeta ritimo riao ande onsi.**

Usidhani kwamba wewe ndiwe bingwa unayechoma mkuki wako popote.

Muktadha: Mazungumzo haya yalitokea katika mkutano ambapo mshauri alitoa onyo kwa washauriwa wanaume dhidi ya kujiona bingwa kwa kufanya ngono kiholela

Matumizi ya fumbo hili ni onyo kwa wanaume wasifanye ngono kiholela. Sehemu ya siri ya mwanaume inalinganishwa na mkuki, ambao ni silaha inayotumiwa wakati wa vita. Fumbo hili linatokana na kitendo cha ngono kulinganishwa na kitendo cha kuchoma mkuki kwa vile katika hali hizo zote kuna kuchoma au "kudunga". Aidha, matumizi ya mafumbo katika mawasiliano kama haya hupunguza aibu ambayo kutumia maneno halisi kutaja sehemu ya siri ya mwanaume ingeleta

washiriki katika mawasiliano huteua lugha mwafaka ili kuepuka aibu katika mazungumzo hayo.

**Ekaramu** na **epensiri** ni mafumbo yanayotokana na maneno ya mkopo, yaani kalamu na penseli. Matumizi ya mafumbo hayo hutoa taswira ya sehemu ya siri ya mwanamke ikiwa kama kitabu nayo sehemu ya mwanaume ikichukuliwa kama kalamu ama penseli ambayo inafanya shughuli ya kuandika. Mafumbo hayo pia yalitumiwa katika hali ya kutoa onyo kwa wanawake na wanaume. Kwa mfano, mwanaume alionywa dhidi ya kuruhusu kalamu (uume) wake kuandika kitabu (uke) chochote, nao wanawake wakionywa kuhusu kuruhusu kila 'kalamu' kuandika 'vitabu' vyao.

Mafumbo haya yalidhihirisha kwamba mwili wa mwanadamu unaweza kutumika katika kuonesha tofauti za kijinsia zilizoko katika mfumo wa jamii ya Abagusii. Githinji (2008) anadai kwamba, maneno yanayotumiwa kutaja sehemu ya siri hudhihirisha umuhimu unaowekwa kwa sehemu hiyo. Anaendelea kusema kwamba, lugha inaweza kutumika katika kukolezea mifumo ya kijamii inayowaonea wanawake na kuwainua wanaume.

Mafumbo haya ya sehemu za siri za mwanaume yanadhihirisha nguvu za wanaume zinazoambatana na heshima na ugumu wao. Vilevile, matumizi ya mafumbo katika kutaja sehemu hizi kunapunguza aibu inayoweza kuletwa na kutumia neno halisi, yaani **emboro** (mboo), au **ekemincha** (mkia). Aidha, inaafikiana na maoni ya Cain na wenzake (2011) kwamba lengo la wazungumzaji katika mawasiliano ni kutumia lugha inayopunguza aibu kwa wasikilizaji.

**Mafumbo kuhusu Sehemu ya Siri ya Mwanamke**

Sura hii inachanganua jumla ya mafumbo 12 yanayoelezea sehemu ya siri ya wanawake. Jedwali lifuatalo linaonesha

orodha ya mafumbo hayo ambapo yamegawanywa katika kategoria mbili, yaliyotokana na vitu vya kiasilia na yaliyotokana na vitu ambavyo kiasilia havikuwepo katika jamii ya Abagusii.

**Mafumbo kuhusu Sehemu ya Siri ya Mwanamke**

| | Maana/ tafsiri | Mafumbo ya kigeni | Maana/ tafsiri |
|---|---|---|---|
| **Obokungu** | Uke | **Egetabu** | Kitabu |
| **Egesima** | Kisima | **Parepare** | pale pale |
| **Ensooko** | Chemichemi | **Ekatiba** | Katiba |
| **Omochie** | Mji | | |
| **Omogondo** | Shamba | | |
| **Egeticha** | kishamba kidogo | | |
| **Ekonu** | Kinu | | |
| **Oboke** | Asali | | |
| **Enyongo** | Mtungi | | |
| **Enyiborero** | ya kuzalia | | |

Chanzo: Utafiti (2017).

Ilibainika kwamba ingawa kuna majina halisi ya kutajia sehemu ya siri ya mwanamke, yaani **embere, egesono** au **ekebenda,** majina haya hayakutumiwa kutajia sehemu hiyo, hususan katika mikutano ya unasihi wa VVU. Badala yake, mafumbo kama vile **obokungu** (uke), **ensooko** (chemichemi) au **enyiborero** (ya kuzalia) yalitumiwa. Kwa Mujibu wa Akama na Maxon (2006), hali hii ilitokana na **chinsoni** (sheria za heshima) zinazowazuia Abagusii kutaja maneno yanayohusu ngono na sehemu za siri kwa lugha wazi. Vilevile, hali hii inaambatana na maoni ya Cain na wenzake (2011) wanaodai kwamba, katika mazungumzo kuhusu dhana ambazo ni mwiko, washiriki huteua maneno mwafaka ili kupunguza aibu.

Sehemu kubwa ya mafumbo yaliyotumika kutaja sehemu ya siri ya mwanamke yanaipa sehemu hiyo jukumu la kutimizia mwanaume haja kama vile kukata kiu yake au kumlisha. Kwa mfano, **ensooko** (chemchemi) na **egesima** (kisima) yote yanatambulisha ile hali sehemu ya siri ya mwanamke kuwa kama maji ambayo yanatumika katika kukata kiu ya mwanaume. Zaidi, mafumbo haya yalitumiwa katika kuonya wanaume dhidi ya kufanya ngono kiholela kama mfano ufuatao unavyoonyesha.

| | |
|---|---|
| Msh: | **Ase twaikeire, mbuya kera omonto konywa amache y'ensoko yaye.**<br>Mahali tumefika sasa, ni vyema kwa kila mtu kunywa maji ya chemchemi yake. |
| Muktadha: | Mazungumzo haya yalitokea katika mkutano ambapo mshauri aliwaonya washauriwa kuhusu hatari ya kufanya ngono kiholela. |

Katika mfano huu, **ensoko** (chemchemi) imetumika kurejelea sehemu ya siri ya mwanamke na kitendo cha kufanya ngono kinalinganishwa na kunywa maji (**konywa amache**). Onyo hili linawalenga zaidi wanaume. Fumbo hili limetokana na mazingira ya wazungumzaji, yaani eneo la Gusii ambalo lina chemichemi nyingi za maji. Hii inaafikiana na maoni ya Steen (2008) kwamba mafumbo hutokana na mazingira ya wazungumzaji.

**Omogondo** (shamba) na **egeticha** (shamba dogo) pia ni mafumbo yaliyotokana na mazingira ya wazungumzaji. Mafumbo haya yanalinganisha sehemu ya siri ya mwanamke na shamba ambalo linatumika katika kuzalisha chakula kinachotumika katika kulisha jamii yote. Matumizi ya mafumbo haya yalifananisha sehemu ya siri ya mwanamke na shamba; ile ya mwanaume ikalinganishwa na jembe ambalo hutumika kupalilia au kulima shamba hilo. Mafumbo haya

a wakati wa kuelezea jinsi ya kutumia kondomu kama
uatao unavyodhihirisha:

h: **Otarasoa mogondo korema, goika obeke chibuti egere tobetwa amagwa.**
Kabla ya kuingia shambani, lazima uvae buti ili usidungwe na miiba

ktadha: Mazungumzo haya yalitokea katika mkutano ambapo mshauri alifafafanua jinsi ya kutumia kondomu katika kujikinga na maambukizi ya VVU.

no huu, fumbo **omogondo** limetumika kurejelea siri ya mwanamke, kitendo cha kufanya ngono hwa na kulima (**korema**), kondomu imeitwa i) navyo VVU vimefanaishwa na miiba (**amagwa).** unadhihirisha jinsi ngono na sehemu za siri zilivyo o hazijadiliwi kwa lugha wazi, bali kwa kutumia yakoe (2011) anadai kwamba, tasfida na mafumbo ayo lugha ya Ekegusii hutumia katika kujadili nbayo ni mwiko kama vile ngono, baadhi ya wili na vile vile haja za kibaolojia za binadamu.

**yiborero** (sehemu ya kuzalia) na **obokungu** (uke) fafanua sehemu za siri za wanawake, hasa wakati insi ya kutumia kondomu. Katika kutumia fumbo nadhihirika wazi kwamba jukumu la sehemu hiyo no ufuatao unadhihirisha hoja hii:

**Ekero kwabeire ang'e koumerana kemobere, okobwata ekondomu eye iga, kwayesoia gochia nyiborero ime.**
Unapokuwa karibu kukutana kimwili, unashika hii ondomu hivi, unaiingiza ndani ya sehemu ya kuzalia.

ambapo mshauri aliwaeleza wanawake manufaa ya kutumia kondomu yao badala ya kutegemea wanaume kuvaa.

Katika mfano huu, ni wazi kuwa jukumu la sehemu hiyo ni kuzaa. Inakuwa rahisi kwa mshauri kutumia fumbo **enyiborero** (ya kuzalia) kuliko kusema **kwayesoia gochia embere ime** kwa vile tamko hili linaondoa aibu ambayo ni lengo kuu la uteuzi wa lugha katika mawasiliano (Cain, 2011). Matumizi ya **enyiborero** (ya kuzalia) ni kisawe cha **obokungu** (uke) kwa vile matumizi yake yanampa mwanamke hadhi fulani. Dhana **obokungu** (uke) imetokana na neno **omokungu** (mwanamke) na ina maana mbalimbali. Maana ya kwanza ni mwanamke aliyekeketwa. Maana hii inamtofautisha **omokungu** na **egesagane** (msichana ambaye hajakeketwa). Kwa hiyo, **obokungu** ni utu uzima. Maana nyingine ya **omokungu** ni mwanamke ambaye ameolewa.

Jamii ya Abagusii huwapa wanawake walioolewa hadhi tofauti na wanawake ambao hawajaolewa. Ni kana kwamba kitendo cha ngono huruhisiwa kutendwa tu na wanawake walioolewa. Kwa hiyo, **omokungu** (mwanamke) ndiye anaruhusiwa kutumia **obokungu** (uke) katika suala la ngono, si ajabu basi kwamba washauri walitumia fumbo hili katika mazungumzo kuhusu VVU/UKIMWI. Mbali na hadhi ambayo matumizi ya mafumbo hayo yanampa mwanamke, matumizi yake (mafumbo) yanapunguza aibu katika mazungumzo, na hili ndilo lengo la uteuzi mwafaka wa lugha (Cain na wenzake, 2011).

Kama tulivyoona, mafumbo kuhusu sehemu ya siri ya mwanamke yanaonesha majukumu mbalimbali ambayo sehemu hiyo huyatekeleza. Miongoni mwayo ni kukata kiu (**ensooko** na **egesima**), kuzaa (**enyibirero**) na kulimwa (**egeticha** na **omogondo**).

## lafumbo kuhusu Kondomu

azungumzo kuhusu VVU/UKIMWI hayawezi kukamilika a kutaja kondomu kama njia ya kupunguza maambukizi. hemu hii inachanganua jumla ya mafumbo 6 ya kuelezea ndomu katika Ekegusii, yote yakiwa yametokana na maneno mkopo. Kondomu ni kifaa ambacho kiasili hakikupatikana ika jamii za Kiafrika. Jedwali lifuatalo linaonesha mafumbo o:

### fumbo Kuhusu Kondomu

| afumbo | Maana/tafsiri |
|---|---|
| **sogisi** | Soksi |
| **gabana** | Kidhibiti mwendo |
| **outi** | Buti |
| **idi** | Cd |
| **opia** | Kofia |
| **nopira** | Mipira |

Chanzo: Utafiti (2017).

ana na mafumbo haya, mielekeo inayojitokeza kuhusu mu wa kondomu katika kuzuia maambukizi inadhihirika. **egaabana** (*governor*) linaichukulia kondomu kama kinachoweza kuokoa maisha ya mtu kwa kupunguza ya VVU. Fumbo hili limetokana na dhana ya eza '*speed governor*', kwa maana ya kifaa wekwa katika magari ili kuthibiti kasi ya gari, na hivyo ajali za barabarani. Fumbo **egaabana** (*governor*') ka kwa kulinganisha kitendo cha ngono na hali ya na gari ambapo inabidi kasi ipunguzwe ili kuepukana Maana inayojitokeza katika matumizi ya fumbo hili ni kuambukizwa na VVU ni sawa na kupata ajali i, kwa hivyo njia ya kuzuia ajali ni kutumia a (*governor*), yaani kondomu. Mbali na kuonesha wa kutumia kondomu, matumizi ya fumbo **egaabana**

(*governor*) yanapunguza aibu ya kuelezea kuhusu kifaa hicho, na hilo ndilo lengo la uteuzi mwafaka wa lugha.

Mafumbo ya **ebuti** (buti) na **esogisi** (soksi) yanafananisha sehemu ya siri ya mwanaume na mguu ambao huvishwa **esogisi** (soksi) au **ebuti** (buti). Hata hivyo, matumizi ya **ebuti** (buti) yanaleta dhana ya kujikinga dhidi ya hatari fulani. Hii ni kwa vile **ebuti** (buti) ni aina ya viatu ambavyo huvaliwa wakati mtu anaenda shambani ili asidungwe na miiba ama wakati wa matope ili mtu asiteleze wala kuchafuka miguu. Kwa hiyo, matumizi ya fumbo **ebuti** hulinganisha sehemu ya siri ya mwanamke na shamba lenye matope au miiba ambayo inaweza kumdhuru mwanaume. Katika muktadha huo, mwanaume anapaswa kujikinga kama mfano ufuatao unavyodhihirisha:

Msh: **Otarasoa mogondo korema, goika obeke chibuti egere tobetwa amagwa**.
Kabla ya kuingia shambani kulima, lazima uvae buti ili usidungwe na miiba.

Muktadha: Mazungumzo haya yalitokea katika mkutano ambapo mshauri alifafanua jinsi ya kutumia kondomu katika kujikinga na maambukizi ya VVU.

Hapa, kondomu imelinganishwa na **chibuti** (buti), viatu ambavyo mtu huvaa wakati anaenda shambani ili kuepuka kuchafuka miguu au kudungwa na miiba. Aidha, matumizi ya fumbo hili yamerahishisha kufanyika kwa mjadala kuhusu matumizi ya kondomu bila kuleta aibu miongoni mwa washiriki. Fumbo **esogisi** (soksi) nalo lilitumiwa kuwasisitiza wanaume kuhusu umuhimu wa kutumia kondomu, hasa wanapofanya ngono na wanawake wasiojua hali zao za VVU. Mfano ufuatao unadhihirisha hili:

Msh: **Kamorache abasacha more aiga, timogoita mokungu onde bwensi biranya,**

**ense yabeire bobe; Korende kerabetererie, beka esogisi gaki.**
Tafadhalini wanaume wote mlioko hapa, msichape mwanamke yeyote viboko, nchi imeharibika; ikibidi, vaa soksi tafadhali.

Muktadha: Mazungumzo haya yalitokea katika mkutano ambapo mshauri aliwaonya wanaume dhidi ya kufanya ngono kiholela na kwamba ikibidi watumie kondomu.

Hapa, fumbo **esogisi** (soksi) limetumika kutaja kondomu ya wanaume. Mshauri huyu anaamua kupunguza aibu katika mazungumzo kwa kutumia fumbo **esogisi** badala ya kutaja neno halisi, **ekondomu** (kondomu).

Ellis (1999) anasema kwamba, matumizi ya mafumbo katika kueleza magonjwa na hali nyinginezo katika lugha za Kiafrika yanaweza kusababisha kutoeleweka kwa ujumbe unaopitishwa. Kwa mfano, fumbo **ebuti** lilitumika kurejelea kondomu inayovaliwa na wanaume na wala sio ile inayovaliwa na wanawake. Kwa hiyo, linaweza kueleweka vibaya, hasa na wanawake, kwa wakilifasiri kuwa wao ndio hatari ambayo wanaume wanapaswa kujikinga dhidi yake. Hata hivyo, katika hali hii, mafumbo hayo yanatumika ili kupunguza aibu katika mazungumzo ya VVU/UKIMWI.

Ujumbe usiokusudiwa vilevile unaweza kupokelewa kutokana na matumizi ya mafumbo yanayolinganisha kondomu na vitu vya kawaida kama vile **ekobia** (kofia) na **esogisi** (soksi). Mafumbo haya yanaweza kufanya kondomu hizo kuchukuliwa kama vitu vya kawaida tu ambavyo havina umuhimu sana katika maisha ya mtu; bila shaka, huo sio ujumbe unaokusudiwa kupitishwa na washauri kama katika mfano ufuatao:

Msh: **Gaki abaminto, tiga omogaka obeka**

**egopia, tagosoka isiko bosa!**
Tafadhalini wenzangu, acha mzee avae
kofia, asitoke nje bila!

Muktadha: Mazungumzo haya yalitokea katika mkutano ambapo mshauri alilinganisha kondomu na kofia.

Hapa, mshauri amelinganisha kondomu na **egopia** (kofia) ambayo huvaliwa kichwani. Kuna hatari ya washiriki kuichukulia kondomu kama kifaa cha kawaida, hivyo kupuuza umuhimu wake. Hata hivyo, kutumia mafumbo katika mijadala kuhusu VVU/UKIMWI kunawawezesha washiriki kuchangia mazungumzo bila kuzua aibu, na hilo ndilo lengo kuu la mawasiliano kama haya.

Steen (2008) anadai kwamba, mojawapo ya majukumu ya mafumbo ni jukumu la kiisimu, yaani kuongezea msamiati katika lugha husika. Matumizi ya fumbo **esidi** (CD) na **egaabana** *(governer)* yanatekeleza jukumu hili. Ingawa maneno haya yana maana yake ya kawaida, maana hiyo imepanuliwa na kuongezwa maana nyingine, yaani kondomu. Kwa hiyo, msamiati wa lugha ya Ekegusii umeweza kupanuka. Kutokana na mifano hiyo ya mafumbo kuhusu kondomu, tumeona kwamba mafumbo hutungwa kulingana na majukumu ambayo kifaa hicho kinadhaniwa kuyatenda. Majukumu hayo ni pamoja na kuzuia ajali, kupunguza ukali wa jua, kuzuia kudungwa. Hata hivyo jukumu kuu ambalo matumizi ya mafumbo yalitekeleza ni kupunguza aibu katika mijadala ya masuala nyeti; na, kwa hakika, hilo ndilo lengo kuu la uteuzi mwafaka wa lugha katika mazungumzo.

## Mafumbo kuhusu Ngono

Jamii mbalimbali hutumia tasfida na mafumbo katika kujadili kitendo cha kufanya ngono. Moto (2004) anatoa mfano wa

tasfida na mafumbo kutoka katika Chichewa, lugha inayozungumzwa nchini Malawi. Anasema kuwa, ngono hutajwa kwa mafumbo kama vile **chikole** (kushika) na **chibwenzi** (kufanya urafiki). Mafumbo katika Sheng kuhusu ngono ni pamoja na kupeana, kuonwa kando, kusuguana, kuandika, kutibiana na kadhalika (Ogechi, 2006). Kadhalika, katika jamii ya Abagusii lugha ya ngono ni mwiko, kwa sababu hiyo mijadala inapofanywa kuhusu suala hilo, hasa inapofanywa hadharani, lugha ya mafumbo na tasfida hutumiwa (Nyakoe, 2011). Sehemu hii inawasilisha jumla ya mafumbo 24 yanayotumiwa kuelezea kitendo cha ngono kama yalivyooneshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 10: Mafumbo kuhusu ngono**

| Mafumbo | Maana/tafsiri |
|---|---|
| **korema omogondo** | kulima shamba |
| **koburuga egeticha** | kupalilia kijishamba |
| **konywa amache** | kunywa maji |
| **goita omokungu ebiranya** | kumchapa mwanamke viboko |
| **koumerana kemobere** | kukutana kimwili |
| **koba n'omokungu/ omosacha** | kuwa na mke au mume |
| **kogendia egari** | kuendesha gari |
| **goaka omopira** | kucheza mpira |
| **koegwa endagera y'abagaka** | kupewa chakula cha wazee |
| **goikerania enyangi** | kutimiza ndoa |
| **konywa amabeere** | kunywa maziwa |
| **komeena oboke** | kulamba asali |
| **goaka egento** | kupiga kitu |
| **gokora emeremo** | kufanya kazi |
| **komanyana kemobere** | kujuana kimwili |
| **Gotaara** | kutembea |
| **gocharoka** | uruka |
| **Koriina** | kupanda |
| **koriana** | kulana |
| **koria egento** | kula kitu |

| | |
|---|---|
| **Komanyana** | kujuana |
| **kogenda n'omonto** | kwenda na mtu |
| **Goswaga** | kutwanga (kwa kinu) |
| **gosoma ekatiba** | kusoma katiba |

Chanzo: Utafiti (2017).

Sehemu kubwa ya mafumbo yaliyotumiwa kujadili ngono yanamweka mwanaume kama mtendaji, huku mwanamke akiwekwa kama mtendewa. Kwa mfano, katika fumbo **korema omogondo** (kulima shamba) mwanaume ndiye mwenye **obokombe** (jembe), ambalo anatumia katika **korema** (kulima). Hali hiyo inadhihirika vile vile katika mafumbo **koburuga egeticha** (kupalilia kishamba kidogo cha mboga) na **kogendia egari** (kuendesha gari) ambapo mwanamke anawekwa katika hali ya mtendewa naye mwanaume anakuwa mtendaji. Mfano ufuatao unadhihirisha hili:

Msh: **Otarasoa mogondo korema, goika obeke chibuti egere tobetwa amagwa**.
Kabla ya kuingia shambani kulima, lazima uvae buti ili usidungwe na miiba.

Muktadha: Mazungumzo haya yalitokea katika mkutano ambapo mshauri alifafanua jinsi ya kutumia kondomu katika kujikinga na maambukizi ya VVU.

Katika mfano huu, kitendo cha kufanya ngono kimerejelewa kwa fumbo **korema omogondo** (kulima shamba). Tamko hili liliwalenga wanaume, kwa vile wanaambiwa wavae **chibuti** (buti) ili 'wasidungwe na miiba wakiwa wanalima shambani'. Fumbo hili linamfananisha mwanamke na shamba ambalo linalimwa. Hata hivyo, kutumia fumbo hili kunarahisisha mjadala kuhusu ngono kufanywa bila kusababisha aibu. Aidha, hupunguza aibu. Mafumbo haya yote yanatumia vitu ambavyo vinafahamika na washiriki katika mazungumzo hayo, kama

vile **omogondo** (shamba), **egeticha** (kishamba kidogo cha mboga) na **egari** (gari). Hivi vyote ni vitu vinavyofahamika na washiriki katika mazungumzo.

Tofauti inaonekana katika mafumbo **koriana** (kulana) na **goaka omopira** (kucheza mpira) ambapo tunawaona wanawake na wanaume katika hali ya washiriki wenza katika kitendo cha ngono. Katika fumbo **koriana** (kulana), kuna taswira ya watu wawili wakilana; hivyo hakuna hali ya mtu mmoja kuwa mpokezi wa kitendo hicho. Hii ni sawa na fumbo **goaka omopira** (kucheza mpira) linaloshirikisha watu kwa viwango sawa. Matumizi ya mafumbo haya hayamweki mwanamke kama mtendaji, bali ni mshirika mwenza katika kitendo cha ngono.

Fumbo **koa omokungu ebiranya** (kumpa mwanamke viboko) linanganisha kitendo cha ngono na adhabu fulani ambayo mwanaume anapaswa kumpa mwanamke. Mfano ufuatao unadhihirisha:

Msh: **Kamorache abasacha more aiga, timogoita mokungu onde bwensi biranya, ense yabeire bobe. Korende kerabetererie, beka esogisi gaki.** Tafadhalini wanaume wote mlioko hapa, msichampe mwanamke yeyote viboko, nchi imeharibika; ikibidi, vaa soksi tafadhali.

Muktadha: Mazungumzo haya yalitokea katika mkutano ambapo mshauri aliwaonya wanaume dhidi kuchapa mwanamke yeyote viboko na kwamba ikibidi watumie kondomu.

Mfano huu unaonesha unyonge wa mwanamke, kwamba yeye ni mpokezi wa viboko kutoka kwa mwanaume (yeye ni mtendewa katika kitendo cha ngono). Kutumia fumbo **goita**

**omokungu ebiranya** (kumchapa mwanamke viboko) kunamwonesha mwanamke kama mnyonge na asiyekuwa na haki ya kufanya uamuzi kuhusu hata mwili wake. Fumbo hili linakoleza dhana kwamba lugha kama mifumo mingine ya kijamii hutumiwa katika kumkandamiza mwanamke na kumweka katika hali ya unyonge na udhaifu (Erkert na Mc Connell-Ginnett, 2006). Hata hivyo, katika muktadha huu, matumizi ya fumbo hili ni mwafaka kwa vile yanasaidia katika kupunguza aibu katika mawasiliano ya suala ambalo ni mwiko.

Fumbo ambalo linaifanya ngono kuonekana kama kitu kizuri au kitamu ni **komena oboke** (kulamba asali). **Oboke** (asali) ni chakula kitamu sana kinachotengenezwa na nyuki. Kulinganisha kitendo cha ngono na kulamba asali kunasawiri dhana ya utamu. Vilevile, kutumia fumbo hilo katika kutaja kitendo cha ngono kunaondoa aibu ambayo ingeletwa kama yangetumika maneno kama vile **gotetena** (kutombana) au **gokorana** (kufanyana). Mfano uliopo hapa chini unaonesha:

| | |
|---|---|
| Msh: | **Ekero okomena oboke, ngwansa bore gose tobori gwansa?**<br>Unapolamba asali, ni tamu au si tamu? |
| Muktadha: | Mazungumzo haya yalitokea katika mkutano ambapo mshauri alilinganisha kitendo cha ngono na kulamba asali. |

Katika mfano huu, hakuna kurejelea mtenda au mtendewa; hivyo, yaelekea kitendo hicho hufurahiwa na washiriki wote. Kutumia fumbo hili **komena oboke** (kulamba asali) kunapunguza aibu wakati wa kuelezea kitendo cha ngono.

Mafumbo mengine ambayo yalitumika na washiriki ni **koba no'monto** (kuwa na mtu) na **gotara** (kutembea). **Koba no'monto** (kuwa na mtu) ni fumbo ambalo hutumiwa hata